Informasjon til deg som har tatt koronatest
Språk: Swahili
Opprettet: 11.2020 Oppdatert: 28.03.2021

NIPH
Norwegian Institute of Public Health

Ukiwa umepimwa virusi vya korona (vipimo vya COVID-19)

Ukipimwa virusi vya COVID-19, inaweza kuchukua siku chache kabla ya kupata majibu. Wasiliana na daktari wako ukiwa mgonjwa au ikiwa unahitaji huduma za matibabu wakati unasubiri majibu yako.

Yeyote anayeshuku kuwa huenda ameambukizwa virusi vya korona anapaswa kupimwa haraka iwezekanavyo. Dalili za kawaida sana ni kupanda kwa joto mwilini/homa, kukohoa, kuumwa na kichwa, kuwashwa koo, matatizo ya kupumua au kupoteza hisia za ladha au harufu. Baadhi ya watu hupata dalili kali zaidi na wengine huenda wasitambue kuwa wameambukizwa.

Unapaswa kupimwa ikiwa uko kwenye karantini, ikiwa uliarifiwa na programu ya Smittestopp au ikiwa huenda umekaribiana na mtu aliyeambukizwa.

Unapaswa kufanya nini wakati unasubiri majibu yako?

Watu wengi ambao wamepimwa wanapaswa kukaa nyumbani au wawe kwenye karantini, wakati wanasubiri majibu ya vipimo. Hupaswi kuenda kazini au shuleni, hupaswi kutumia usafiri wa umma na hupaswi kuenda kwenye maeneo ya umma. Unapaswa kukaa mbali na kila mtu, ikiwa ni pamoja na watu wazima na watoto walio na umri mkubwa ambao unaishi nao. Watoto wadogo wanapaswa kutunzwa kama kawaida.

- **Ikiwa ulipimwa kwa sababu una dalili za virusi vya korona,** unapaswa kukaa nyumbani na kukaa mbali na watu wengine wakati unasubiri majibu yako ya vipimo.
- **Ikiwa ulipimwa kwa sababu ulikaribiana na aliyeambukizwa au uliarifiwa na programu ya Smittestopp**, unapaswa kukaa nyumbani wakati unasubiri majibu yako ya vipimo.
- **Ikiwa uko kwenye karantini ya lazima ya walioambukizwa**, unapaswa kupimwa unapoanza kukaa karantini na kupimwa tena kabla ya kipindi cha kukaa karantini kumalizika. Kukaa karantini kunahitajika kisheria na unaweza kupigwa faini ikiwa utakaidi. Watu unaoishi nao lazima wakae kwenye karantini ya kusubiri hadi utakapopokea majibu ya vipimo vya kwanza yanayoonyesha kuwa hujaambukizwa. Ni lazima uendelee kukaa karantini katika kipindi hiki. Unapaswa kupimwa tena baada ya siku 7 kupita tangu ulipokaribiana na mtu aliyeambukizwa. Ikiwa majibu ya vipimo vya baada ya siku 7 yataonyesha kuwa hujaambukizwa, unaweza kuondoka kwenye karantini. Ikiwa hujapimwa, utaendelea kukaa karantini kwa siku 10 baada ya mara ya mwisho ya kukaribiana na mtu aliyeambukizwa. Ikiwa una dalili, unapaswa kupimwa tena.
- **Ukiwa uko kwenye karantini ya waliowasili** baada ya kuwasili nchini Norwe, unapaswa kupimwa baada ya kuwasili na baada ya siku 7 kamili kupita. Kupimwa na kukaa karantini vinahitajika kisheria na unaweza kupigwa faini ikiwa utakaidi. Ikiwa

majibu ya vipimo vya baada ya siku 7 yataonyesha kuwa hujaambukizwa, unaweza kuondoka kwenye karantini. Ikiwa unaishi na watu wengine na huwezi kudumisha umbali wa kutokaribiana nao, wanapaswa kukaa nyumbani ukiwa kwenye karantini. Ukianza kuonyesha dalili, unapaswa kupimwa tena.

- **Ikiwa uko kwenye karantini ya lazima na ulipimwa kwa sababu una dalili za virusi vya korona,** unapaswa kufuata sheria za kujitenga kwa sababu kuna uwezekano kuwa umeambukizwa COVID-19. Sheria za kujitenga ni kali zaidi kuliko zile za kukaa karantini. Watu unaoishi nao wanapaswa kukaa karantini hadi utakapopokea majibu ya vipimo vyako vya kwanza. Watu unaoishi nao wanaweza pia kuhitaji kupimwa.
- **Ikiwa ulipimwa hata kama huna dalili za virusi vya korona na hujakaribiana na aliyeambukizwa**, huhitaji kukaa nyumbani hadi utakapopokea majibu yako ya vipimo. Masharti haya yanatumika, kwa mfano, ikiwa ulipimwa kwa sababu unashiriki katika mradi wa utafiti, unaenda kutembelea taasisi fulani au ikiwa unapaswa kupimwa ndipo uweze kusafiri.

Jinsi ya kupata majibu yako ya vipimo

Baada ya karibu siku 1 hadi 2, utaweza kupata majibu ya vipimo vyako vya virusi vya korona katika Helsenorge.no (https://www.helsenorge.no/en/test-results/). Wakati mwingine inaweza kuchukua muda mrefu kiasi.

Yeyote aliye na kitambulisho cha kitaifa cha Norwe au D-number ambaye ana nambari ya simu iliyosajiliwa au anwani ya barua pepe chini ya maelezo ya Mawasiliano (“Kontaktinformasjon”) katika helsenorge.no ataarifiwa kwa ujumbe mfupi au kwa barua pepe majibu yakiwa tayari. Ikiwa huna kitambulisho cha kitaifa cha Norwe au D-number, ni lazima uwasiliane na kituo cha upimaji ambapo ulipimwa au huduma ya usaidizi wa virusi vya korona katika manispaa yako ili upate majibu yako.

Ikiwa una virusi vya korona, majibu yataonyesha kuwa umeambukizwa au amethibitishwa (“positivt/påvist”). Ikiwa huna virusi vya korona, majibu yataonyesha kuwa hujaambukizwa au hajathibitishwa (“negativt/ikke påvist”).

Ikiwa vipimo vitaonyesha kuwa una virusi vya korona (majibu ya vipimo yanayoonyesha kuwa umeambukizwa)

Ikiwa vipimo vitaonyesha kuwa una COVID-19 (virusi vya korona), ni lazima ujitenge. Timu ya ufuatiliaji wa waliokaribiana na aliyeambukizwa ya manispaa yako itawasiliana nawe.

Shughuli ya ufuatiliaji wa waliokaribiana na aliyeambukizwa ni muhimu katika kukomesha kusambazwa kwa maambukizi. Kwa hivyo, ni lazima watu wote waliokaribiana nawe (kila mtu unayeishi naye na kila mtu uliyekaribiana naye) wakae karantini. Wanapaswa pia kupimwa.

Manispaa ina jukumu la kudumisha faragha ya kila mtu. Ni muhimu kuelewana, kwa hivyo ni lazima uulize maswali ikiwa huna uhakika kuhusu jambo lolote. Unaweza kuomba kupata huduma za mkalimani ikiwa ni vigumu kuelewa lugha inayotumika. Huduma ya mkalimani hailipishwi.

Manispaa inaweza kukusaidia kupata mahali pengine pa kuishi ikiwa huwezi kudumisha umbali wa kutokaribiana na watu unaoishi nao ukiwa umejitenga.

Sheria na ushauri kuhusu kukaa karantini na kujitenga

- Sheria na ushauri kuhusu kukaa karantini na kujitenga: https://www.fhi.no/en/op/novel-coronavirus-facts-advice/facts-and-general-advice/social-distance-quarantine-and-isolation/
- Sheria na ushauri kuhusu kukaa karantini na kujitenga vimetafsiriwa pia kwa lugha nyingi https://www.fhi.no/en/op/novel-coronavirus-facts-advice/information-material/informasjon-different-languages/
- Chini ya sheria ya sasa, kuvunja sheria za kukaa karantini na kujitenga linaweza kuchukuliwa kama kosa la uhalifu.